# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA VILEO, SURA YA 163 YA MWAKA 1928 NA KUTUNGA SHERIA INAYOWEKA MASHARTI YA KUDHIBITI NA KUSIMAMIA UAGIZAJI, UHIFADHI, UUZAJI, USAMBAZAJI NA UNYWAJI VILEO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Matumizi.
3. Ufafanuzi.
4. Marufuku kutengeneza na kuzalisha vileo.
5. Marufuku kunywa au kukutwa na vileo.
6. Leseni za kuuza na kuweka kwenye ghala za vileo.
7. Kibali cha Uagizaji na Usambazaji vileo.

**SEHEMU YA PILI**
**UANZISHWAJI WA BODI YA KUDHIBITI VILEO ZANZIBAR**

8. Kuanzishwa kwa Bodi.
9. Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.
10. Kujiuzulu kwa Mwenyekiti au mjumbe.
11. Katibu wa Bodi.
12. Uwezo na majukumu ya Bodi.
13. Kamati za Bodi.
14. Kukasimu kazi za Bodi.
15. Vikao vya Bodi.

16. Akidi ya kikao cha Bodi.

17. Maamuzi ya Bodi.

18. Kumbukumbu za Bodi.

19. Taratibu za vikao vya Bodi.

20. Kufungwa kwa duka la vileo, baa au klabu.

21. Pingamizi.

22. Bodi inaweza kuzuia.

23. Posho za Wajumbe.

24. Ripoti ya mwaka.

**SEHEMU YA TATU**
**LESENI, VIBALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO**

25. Leseni na vibali vinavyoweza kutolewa.

26. Ombi la Leseni au Kibali.

27. Kufanya maombi mapya.

28. Masharti ya utoaji wa leseni.

29. Leseni ya hoteli.

30. Leseni ya baa.

31. Leseni ya duka la vileo.

32. Leseni ya ghala.

33. Kibali cha kuagiza.

34. Kibali cha usambazaji.

35. Utaratibu wa kuhifadhi vileo katika maeneo yaliyoruhusiwa.

**SEHEMU YA NNE**
**UWEZO NA WAJIBU WA MAAFISA**

36. Mkaguzi na Maafisa wa Bodi.

37. Ukaguzi.

38. Matumizi mabaya ya mamlaka.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA


39. Fedha za Bodi.

40. Hesabu na ukaguzi.


## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA ADHABU


41. Makosa ya mtu aliyekatazwa.

42. Makosa ya leseni.

43. Amri ya kuzuia.

44. Watu wasioruhusika kujishughulisha na biashara au muamala wa vileo.

45. Kuuza au kuweka kwenye ghala bila ya leseni.

46. Kutumia nyaraka za uongo.

47. Mahakama kuidhinisha hukumu.

48. Hukumu ya papo kwa papo.

49. Adhabu ya jumla.


## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA


50. Uwezo wa Waziri kutoa maelekezo kwa Bodi.

51. Kinga dhidi ya kushitakiwa.

52. Kanuni.

53. Kufutwa.

**SHERIA NAM. 9 YA 2020**

**NIMESAINI**

Ashein

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

11 Mei ........................................................, **2020**

**SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA VILEO, SURA YA 163 YA MWAKA 1928 NA KUTUNGA SHERIA INAYOWEKA MASHARTI YA KUDHIBITI NA KUSIMAMIA UAGIZAJI, UHIFADHI, UUZAJI, USAMBAZAJI NA UNYWAJI VILEO NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO**

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina Fupi na Kuanza Kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kudhibiti Vileo, 2020 na itaanza kutumika baada ya kutiwa saini na Rais.

Matumizi.

**2.**-(1) Sheria hii itatumika kwa mtu yeyote anayejishughulisha na uagizaji, uhifadhi, uuzaji, usambazaji na utumiaji wa vileo Zanzibar.

(2) Isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo, Sheria hii haitatumika kwa:

(a) spiriti isiyofaa kunywewa;

(b) ulevi usiofaa kunywewa;

(c) marashi, shira na mchanganyiko wa dawa yenye ulevi kwa ajili ya kutengenezea maji na vinywaji vya kuchangamsha mwili;

(d) uagizaji, uuzaji, uchukuaji au utoaji wa dawa, vipodozi, manukato yaliyotengenezwa au yenye mchanganyiko na spiriti, chini ya Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi ya Zanzibar;

(e) daktari au muuza dawa yeyote aliyesajiliwa au mwenye leseni ya kuagiza, kupeleka, kutoa au kuuza dawa yoyote yenye kileo ndani yake kwa ajili ya kutibu; na

(f) mtu yeyote anayefanya kazi chini ya mamlaka iliyoundwa kwa mujibu wa sheria katika kutenda au kutekeleza majukumu yake.

Ufafanuzi.

**3.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama itaelezwa vyenginevyo:

"kileo kilichofanyiwa ghushi" maana yake ni kileo chochote kilichochanganywa au kutiwa maji au kitu chengine chochote, ikiwa ni hatari kwa afya au vyenginevyo, ama ni kwa ajili ya kukiongezea wingi wake au kipimo chake au kubadili ubora wake au kuficha ubora wa kileo hicho;

"ulevi" maana yake ni kinywaji kilichovundikwa au kuzalishwa kwa mvuke wa nafaka, matunda au mazao mengine ya kilimo, ikiwa ni pamoja na mchanganyiko wa vileo vya 'ethyl' vyenye kilevi kinachozidi asilimia 0.5;

"Bodi" maana yake ni Bodi ya Kudhibiti Vileo Zanzibar iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria hii;

"gari la kibiashara" maana yake ni gari au lori lililotengenezwa na linalotumika kwa ajili ya kusafirishia bidhaa za aina yoyote;

"mahakama" inajumuisha Majaji na Mahakimu wote na watu wote wasiokuwa wasuluhishi, walioidhinishwa kisheria kuchukuwa ushahidi;

"usiofaa kunywewa" maana yake ni kuwa haifai kabisa kwa matumizi ya binadamu;

"ulevi usiofaa kunywewa" maana yake inajumuisha ulevi wowote au kinywaji chochote ambacho mchanganyiko wake umepelekea kuwa hakifai kwa matumizi kama kinywaji;

"spiriti isiyofaa kunywewa" maana yake ni spiriti yenye 'methyl' na inajumuisha kileo chochote ambacho kwa kuchanganywa na kitu kinapelekea kutofaa kwa matumizi kama kinywaji;

"idara ya Serikali" maana yake ni idara, taasisi, jengo au kitengo chochote cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar au Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hapa Zanzibar;

"mgeni" maana yake ni mtu yeyote ambaye amelipia au kulipiwa, malazi au huduma za chakula, vinywaji au huduma zozote nyengine zilizoidhinishwa ndani ya hoteli;

"hoteli" maana yake ni sehemu, eneo au mahala penye stara, panapoendeshwa na watu wenye sifa nzuri, ambapo mgeni anaweza, baada ya kulipia, kupata sehemu ya kulala, vinywaji na vyakula na ambayo kwa maeneo ya mjini, ina angalau vyumba kumi na katika mahali pengine angalau vyumba sita vya kudumu kwa matumizi ya wageni, eneo la sebule au chumba kwa ajili ya wageni hao ambalo linaweza angalau kuhudumia watu thelathini kwa wakati mmoja na jiko, mbali na sehemu ya kulia chakula ambalo kikawaida linatumika kuandalia chakula;

"kuingiza" maana yake ni kuleta au kuletwa hapa Zanzibar kwa njia ya barabara, baharini au ndege;

"taasisi" maana yake ni idara au taasisi yoyote ya Serikali au za kibinafsi, kituo, jengo au majengo yaliyopo Zanzibar;

"vileo vinavyolewesha" maana yake ni kinywaji chochote kile ambacho kina zaidi ya asilimia 0.5 ya ulevi, lakini haijumuishi pombe ya kienyeji;

"leseni" maana yake ni ruhusa yoyote iliyotolewa chini ya Sheria hii;

"mwenye leseni" maana yake ni mtu yeyote ambaye ana leseni iliyotolewa chini ya Sheria hii;

"majengo yenye leseni" maana yake ni majengo, eneo au mahali popote palipofanyiwa marekebisho ya msingi kwa lengo husika na paliporuhusiwa kwa leseni chini ya Sheria hii;

"ghala yenye leseni" maana yake ni ghala au mahali pengine panaporuhusiwa kuhifadhia vileo vinavyolewesha chini ya Sheria hii;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na masuala ya serikali za mitaa;

"afisa wa Bodi" maana yake ni mtu yeyote aliyeidhinishwa kutenda kazi chini ya Sheria hii;

"kibali" maana yake ni kibali chochote kilichotolewa chini ya Sheria hii;

"Polisi" maana yake ni muajiriwa yeyote wa Jeshi la Polisi mwenye cheo cha au juu ya cheo cha konstebo.

"uchukuaji" maana yake ni udhibiti halisi na inajumuisha mtu kuwa na vileo au uhifadhi wa mtu mwengine kwa matumizi au maslahi yake mwenyewe au ya mtu mwengine yeyote;

"mtu aliyekatazwa" kwa madhumuni ya Sheria hii, maana yake ni gari ya abiria au mtu yeyote ambaye umri wake ni chini ya miaka ishirini na moja au mtu ambaye bado yupo chini ya uangalizi wa wazazi au walezi au mtu ambaye amepigwa marufuku kwa amri ya Mahakama kwa mujibu wa Sheria hii;

"gari ya abiria" maana yake ni gari ambayo hubeba au iliyokusudiwa kubeba abiria kwa nauli;

"manukato yaliyotengenezwa au yenye mchanganyiko wa spiriti" maana yake ni manukato au uturi wowote au dawa ya kusafishia choo yenye mchanganyiko wenye mafuta yenye spiriti;

Marufuku kutengeneza na kuzalisha vileo.

**4.**-(1) Ni marufuku mtu au taasisi yoyote kutengeneza au kuzalisha vileo vinavyolewesha hapa Zanzibar.

(2) Mtu au taasisi yoyote ambayo itakwenda kinyume na masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ni mkosa, na akipatikana na hatia, atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano au atalipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano na vileo vyake vyote pamoja na mashine ya kuzalishia au kutengenezea vileo hivyo zitataifishwa na kushughulikiwa kama Bodi itakavyoelekeza.

Marufuku kunywa au kukutwa na vileo.

**5.**-(1) Mtu aliyekatazwa ni marufuku kwake kunywa au kukutwa na vileo vinavyolewesha vya aina yoyote ile hapa Zanzibar.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kunywa au kumpa mtu yeyote kunywa au kununua au kukutwa na spiriti isiyofaa kunywewa au ulevi usiofaa kunywewa au kukutwa anataka kunywa.

(3) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini au kutumikia kifungo kwa kipindi kilichotajwa katika kifungu cha 42(2) cha Sheria hii.

Isipokuwa kwamba katika kesi yoyote iliyo chini ya kifungu hiki, wajibu wa kuthibitisha kuwa usambazaji au ununuzi huo au kukutwa na ulevi au spiriti isiyofaa kunywewa ilikuwa ni kwa madhumuni mengine yasiyokuwa ya kunywa, utakuwa kwa mtu huyo anayedai hivyo.

Leseni za Kuuza na kuweka kwenye ghala za vileo.

**6.**-(1) Hakuna mtu, idara ya Serikali au taasisi yoyote itakayoruhusiwa kuuza au kuweka vileo vinavyolewesha vya aina yoyote kwenye ghala bila ya kuwa na leseni inayoruhusu uuzaji au uwekaji vileo hivyo ghalani.

(2) Hakuna mtu, idara ya Serikali au taasisi yoyote iliyoruhusiwa kuuza vileo vinavyolewesha kwa jumla au reja reja ambayo itaruhusiwa kutunza au kuhifadhi vileo hivyo kwenye mahali pengine zaidi ya maeneo yatakayoainishwa katika leseni.

Isipokuwa kwamba kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki hakitotumika kwa vileo ambavyo vinataka kupelekwa sehemu nyengine au ni kwa matumizi ya kibinafsi au haviuzwi.

(3) Hakuna mtu anayeruhusika kukutwa na vileo isipokuwa mtu mwenye leseni chini ya Sheria hii au mtu aliyenunua au kupata vileo hivyo, vinavyolewesha kwa ajili ya matumizi yake binafsi na sio kuuza.

(4) Kila mwenye leseni ataibandika au kuipachika leseni yake mahali palipo wazi kwenye eneo linalotumiwa leseni hiyo.

(5) Mtu, idara ya Serikali au taasisi yoyote inayotaka leseni yoyote au kibali au kulipia upya leseni au kibali kwa ajili ya kuuza, kutunza kwenye ghala, kuagiza au kusambaza vileo vinavyolewesha Zanzibar atafanya maombi yeye mwenyewe katika fomu iliyowekwa, kwa kutuma nakala tatu, kwenye Bodi ndani ya muda usiozidi siku saba baada ya kuchapishwa kwa matangazo ya kusikilizwa kwa maombi hayo.

(6) Mtu, idara ya Serikali au taasisi yoyote ambayo imenyimwa kupewa leseni ya kuuza au kutunza vileo vinavyolewesha kwenye ghala au kwamba imekataliwa kufanya upya leseni au kibali chake au leseni yake imefutwa au kubatilishwa kwa sababu yoyote katika Sheria hii, mtu, idara au taasisi hiyo haitopewa leseni hadi itakaporekebisha kasoro zilizobainika na kuomba tena leseni hiyo.

(7) Wakati malipo ya kufanya upya yakikataliwa na Bodi, mwombaji, baada ya malipo ya ada iliyoamriwa, atapewa kibali cha muda maalum kwa kipindi cha kuuza vileo viliyobakia kwenye eneo hilo ndani ya miezi mitatu.

Kibali cha Uagizaji na Usambazaji vileo.

**7.**-(1) Hakuna mtu, idara ya Serikali au taasisi yoyote itakayoagiza au kusambaza vileo vinayolewesha bila ya kuwa na kibali kinachoruhusu uagizaji au usambazaji huo.

(2) Mtu, idara ya Serikali au taasisi yoyote inayotaka kuagiza au kusambaza vileo isipokuwa kama imeelezwa vyenginevyo, itatuma maombi kwenye Bodi kuomba kibali cha uagizaji au usambazaji vileo vinavyolewesha Zanzibar.

## SEHEMU YA PILI
## UANZISHWAJI WA BODI YA KUDHIBITI VILEO ZANZIBAR

Kuanzishwa kwa Bodi.

**8.**-(1) Kutakuwa na Bodi ya Ushauri ya Kudhibiti Vileo Zanzibar ambayo itakuwa na wajumbe wafuatao:-

(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) Mkurugenzi Uratibu Tawala za Mikoa na Serikali za mitaa;

(c) Mkurugenzi anayehusika na utalii;

(d) Wakili wa Serikali mmoja kutoka Afisi ya Mwanasheria Mkuu;

(e) Mwakilishi mmoja kutoka Jeshi la Polisi;

(f) Mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara na Wakulima Zanzibar; na

(g) Mwakilishi mmoja kutoka Jumuiya ya Wafanyabiashara wa Utalii.

(2) Isipokuwa Mwenyekiti na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe wengine watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na taasisi husika kwa kuzingatia uzoefu, uadilifu, taaluma na jinsia.

(3) Mwenyekiti atashikilia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka minne lakini anaweza kuteuliwa tena.

(4) Mjumbe atashikilia nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitatu na anaweza kuteuliwa tena.

(5) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mwenyekiti ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana elimu ya angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria, biashara, uhasibu, utawala au fani nyengine zinazolingana kutoka katika taasisi inayotambulika;

(c) ana uzoefu wa kazi wa kutosha katika fani zilizoelezwa chini ya aya (b) ya kifungu kidogo hiki; na

(d) anaheshimika.

(6) Mjumbe aliyeteuliwa na Waziri chini ya aya za (e), (f) na (g) za kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atasita kuwa mjumbe wa Bodi mara baada ya sifa za uteuzi wake zitakaposita.

(7) Wajumbe wa Bodi katika kikao cha kwanza, watamchagua mjumbe mmoja miongoni mwao kuwa Makamu Mwenyekiti.

Nafasi ya mjumbe kuwa wazi.

**9.** Nafasi ya mjumbe wa Bodi itakuwa wazi, ikiwa mjumbe:

(a) atamaliza muda;

(b) bila ya sababu ya msingi, atashindwa kuhudhuria vikao vitatu mfululizo vya Bodi;

(c) atajiuzulu au kwa sababu yoyote, atapoteza sifa za kuwa mjumbe wa Bodi;

(d) atatiwa hatiani kwa kosa la jinai;

(e) atashindwa kufuata Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii;

(f) hana uwezo wa kutekeleza majukumu yake kutokana na sababu ya afya ya kimwili au kiakili; au

(g) atafariki.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii yanayohusiana na akidi, uendeshaji wa vikao vya Bodi hautokuwa batili kwa sababu ya nafasi kuwa wazi au kutohudhuria kwa mjumbe yeyote wa Bodi.

Kujiuzulu kwa Mwenyekiti au mjumbe.

**10.**-(1) Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi, anaweza kujiuzulu wakati wowote kwa kuandika taarifa ya kujiuzulu na kuiwasilisha katika mamlaka ya uteuzi na kuanzia tarehe iliyoainishwa katika taarifa au ikiwa tarehe haikuainishwa, kuanzia tarehe iliyopokelewa taarifa na mamlaka ya uteuzi, mtu huyo atasita kuwa Mwenyekiti au mjumbe.

(2) Endapo mtu atasita kuwa Mwenyekiti au mjumbe wa Bodi, kama itakavyokuwa, kwa sababu yoyote kabla ya kumalizika kwa muda, mamlaka ya uteuzi itateua mtu mwengine kushika nafasi hiyo na mtu huyo aliyeteuliwa atashika nafasi kwa kipindi kilichobaki cha aliyetangulia.

(3) Endapo mjumbe aliyeteuliwa na Waziri atashindwa kuhudhuria kwenye vikao vitatu mfululizo bila ya sababu ya msingi, Mwenyekiti atamjulisha Waziri kuhusiana na hilo na Waziri atafuta uteuzi wa mjumbe huyo na kuteua mtu mwengine na mtu aliyeteuliwa atashika nafasi hiyo kwa kipindi kilichobaki cha aliyetangulia.

Katibu wa Bodi.

**11.**-(1) Kutakuwa na Katibu wa Bodi atakayeteuliwa na Bodi.

(2) Mtu atakuwa na sifa za kuchaguliwa kuwa Katibu wa Bodi, ikiwa mtu huyo ana angalau shahada ya kwanza katika fani ya sheria, biashara, uhasibu au utawala.

(3) Katibu wa Bodi atawajibika kwa Bodi na atahakikisha kuwa:

(a) kumbukumbu sahihi za vikao zinachukuliwa na kutunzwa kwa umakini;

(b) taarifa sahihi za vikao vya Bodi zinatolewa kwa wajumbe; na

(c) anatoa ushauri sahihi kwa Bodi wakati unapohitajika na mambo mengine kama Bodi itakavyoagiza.

Uwezo na majukumu ya Bodi.

**12.**-(1) Bodi itakuwa na uwezo na majukumu ya:

(a) kudhibiti uuzaji, uagizaji , uhifadhi, utumiaji na usambazaji wa vileo;

(b) kuweka masharti ya utunzaji wa majengo yaliyopewa leseni ya vileo na kudhibiti utunzaji na usambazaji kutoka kwenye maeneo hayo;

(c) kuidhinisha uuzaji, uhifadhi, uwekaji kwenye maghala, usambazaji au utumiaji wa vileo vinavyolewesha;

(d) kuandaa miongozo juu ya ada na tozo zinazohusiana na biashara ya vileo zitakazotozwa na mamlaka ya serikali za mitaa;

(e) kufanya shughuli zote zinazohusiana na usimamizi wa Bodi;

(f) kupendekeza kwa Waziri, kuteuliwa kwa watumishi na maafisa wa Bodi kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii;

(g) kusimamia maombi, utoaji, ulipiaji upya wa leseni na vibali na kumalizika kwa leseni na vibali;

(h) kuweka masharti ambayo yanaambatana na leseni na vibali;

(i) kuweka masharti juu ya vibali maalum vinavyoweza kutolewa;

(j) kufanya ukaguzi katika maeneo ya uuzaji na ghala za kuhifadhia vileo;

(k) kuweka fomu za hati za ununuzi, hati za uuzaji, viwango vya majengo yaliyopewa leseni na majengo yanayotumiwa na wenye leseni au vibali kwa uuzaji na utoaji wa huduma za vileo;

(l) kumshauri Waziri katika utekelezaji mzuri wa udhibiti wa biashara na matumizi ya vileo; na

(m) kwa kushauriana na Waziri, kufanya kitu chochote muafaka katika utekelezaji wa Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Bodi inaweza kufuta au kubatilisha leseni au kibali chochote kwa sababu yoyote ambayo inaweza kumkosesha mtu haki ya leseni au kibali chini ya Sheria hii, ikiwa amekiuka masharti ya Sheria hii, Kanuni au masharti ya leseni au kibali.

Kamati za Bodi.

**13.** Bodi inaweza kuunda kamati kama itakavyoona inafaa.

Kukasimu kazi za Bodi.

**14.** Bodi inaweza, katika utekelezaji bora wa kazi zake, kukasimu baadhi ya kazi zake kwa kamati.

Vikao vya Bodi.

**15.**-(1) Bodi itafanya vikao vyake vya kawaida mara moja katika kila kipindi cha miezi mitatu na inaweza kukutana ikiwa kuna haja ya kufanya hivyo.

(2) Kikao cha Bodi kitaitishwa na kuendeshwa na Mwenyekiti, ikiwa Mwenyekiti hayupo, Makamu Mwenyekiti ataendesha kikao na ikiwa wote wawili hawapo, wajumbe waliopo katika kikao watamteua mmoja miongoni mwao kuendesha kikao.

(3) Bodi inaweza kumualika mtu yeyote kuhudhuria katika kikao chochote cha Bodi kama mtaalamu lakini mtu huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura.

Akidi ya kikao cha Bodi.

**16.** Akidi ya kikao cha Bodi itakuwa ni zaidi ya nusu ya wajumbe wa Bodi.

Maamuzi ya Bodi.

**17.** Maamuzi ya Bodi yatafanywa kwa njia ya makubaliano na ikiwa makubaliano hayatofikiwa, maamuzi yatafanyika kwa kupiga kura na endapo kura zitakuwa sawa, Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti au mjumbe atakayeendesha kikao, atakuwa na kura ya maamuzi.

Kumbukumbu za Bodi.

**18.** Kumbukumbu za uendeshaji wa vikao vyote vya Bodi zitathibitishwa katika kikao kinachofuata cha Bodi na kuwekwa saini na Mwenyekiti wa kikao na Katibu wa Bodi.

Taratibu za vikao vya Bodi.

**19.** Kwa kuzingatia masharti ya Sheria hii, Bodi itakuwa na uwezo wa kuweka taratibu zake zinazohusiana na vikao na uendeshaji bora wa kazi zake ikijumuisha kamati za Bodi.

Kufungwa kwa duka la vileo, baa au klabu.

**20.** Mamlaka ya serikali za mitaa itakuwa na uwezo wa kufunga duka la vileo, baa au klabu itakayokiuka masharti ya Sheria hii.

Pingamizi.

**21.** Endapo itajitokeza pingamizi ya maandishi dhidi ya maombi kutoka kwa wakaazi wa eneo husika, Bodi itazingatia pingamizi hiyo, na:

(a) kupitia upya ombi hilo;

(b) kukubali ombi hilo ikiwa halipingani na masharti ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote; au

(c) kukataa ombi hilo.

Bodi inaweza kuzuia.

**22.** Bodi inaweza, kwa amri iliyochapishwa kwenye Gazeti Rasmi, kueleza idadi ya leseni au vibali vilivyoruhusiwa na vilivyozuiliwa kutolewa katika eneo lolote Zanzibar.

Posho za Wajumbe.

**23.** Mwenyekiti na wajumbe wa Bodi watalipwa kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma, Kanuni na miongozo.

Ripoti ya mwaka.

**24.** Mwenyekiti atatayarisha ripoti ya kila mwaka ya shughuli za Bodi na kuiwasilisha kwa Waziri baada ya tarehe thelathini ya mwezi wa Juni ya mwaka wa fedha na si zaidi ya baada ya siku thelathini.

## SEHEMU YA TATU
## LESENI, VIBALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NAYO

Leseni na vibali vinavyoweza kutolewa.

**25.**-(1)Leseni na vibali vifuatavyo, kulingana na Sheria hii na Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii, vinaweza kutolewa na Bodi baada ya malipo ya ada iliyowekwa:

(a) Leseni ya hoteli;

(b) Leseni ya baa;

(c) Leseni ya duka la vileo;

(d) Leseni ya ghala;

(e) Kibali cha kuagizia vileo;

(f) Kibali cha usambazaji vileo; na

(g) Kibali cha hafla maalum.

(2) Hakuna taasisi au mtu atakayepewa kibali au leseni zaidi ya moja katika eneo moja kwa bidhaa za aina moja.

(3) Bila ya kuathiri masharti yaliyoelezwa katika Sheria hii, leseni au vibali vyote vitakavyotolewa, vitasita kufanya kazi kwa muda wote wa kipindi cha mwezi wa Ramadhani, isipokuwa kwa hoteli zenye hadhi ya kuanzia nyota moja na mikahawa ya kitalii.

(4) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (3) cha kifungu hiki, taasisi au mtu yeyote akifungua baa, klabu, duka la vileo, ghala la vileo au akiuza, akinunua, akitumia, akiagiza au akisambaza vileo ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani atakuwa anafanya kosa na akitiwa hatiani atapewa adhabu kama iliyotajwa katika kifungu cha 42(2) cha Sheria hii.

Ombi la Leseni au Kibali.

**26.**-(1) Maombi ya kibali au leseni yoyote yatafanywa kwa Bodi.

(2) Tofauti na masharti ya vibali, leseni zote zitakuwa kwa kipindi cha miezi kumi na moja na kwa hoteli na mikahawa ya kitalii, itakuwa kwa miezi kumi na mbili.

(3) Leseni zote na vibali vyote vilivyotolewa chini ya Sheria hii vitakuwa katika mfumo uliowekwa.

(4) Bodi, inaweza kuweka mazingira ya kutolewa vibali vya hafla maalum.

Kufanya maombi mapya.

**27.**-(1) Mtu yeyote ambaye ameruhusiwa na Sheria hii au Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii kuendesha biashara ya marehemu aliyekuwa na leseni anaweza, wakati wa kikao kinachofuata cha mwaka cha Bodi, kufanya maombi mapya kama mtu ambaye hakuwa na leseni.

(2) Mtu yeyote ambaye ameruhusiwa na sheria yoyote kuendesha biashara ya mtu mwengine mwenye leseni, atakuwa na haki zote, wajibu, majukumu na dhima zote za mwenye leseni hiyo.

Masharti ya utoaji wa leseni.

**28.** Hakuna leseni ya kuuza au kuhifadhi vileo ghalani itakayotolewa ikiwa:

(a) ukiangalia uwezo wa kifedha wa mwombaji, mwombaji hana uwezo wa kifedha kufanya biashara hiyo;

(b) kutokana na tabia alizonazo mwombaji, kuna kila sababu ya kuamini kwamba mwombaji hatofanya biashara kwa mujibu wa Sheria hii na kwa uadilifu na uaminifu;

(c) mwombaji au mfanyakazi au wakala wa mwombaji atatoa maelezo ya uongo au taarifa ya uongo katika maombi chini ya Sheria hii;

(d) mwombaji anafanya shughuli ambazo ni kinyume na sheria, au anavunja Sheria hii au kanuni, endapo mwombaji atapewa leseni;

(e) mwombaji anafanya shughuli ambazo zinakiuka au zitakiuka sheria yoyote endapo mwombaji atapewa leseni;

(f) majengo, malazi, zana na vifaa ambavyo vinaombewa leseni havikidhi masharti ya Sheria hii au Kanuni zake endapo mwombaji akipewa leseni;

(g) mwombaji akishindwa kuiridhisha Bodi kwamba ataweza kuidhibiti vizuri biashara yake, pamoja na majengo, malazi, zana na vifaa ambavyo anaviombea leseni hiyo;

(h) mwombaji ana sifa na tabia mbaya au tabia za ulevi;

(i) majengo ambayo yanafanywa maombi ya leseni ni machafu na mabovu;

(j) idadi ya majengo yaliyopewa leseni yanatosha katika eneo hilo au manispaa; au

(k) majengo hayo yapo umbali wa chini ya mita elfu moja kutoka maeneo ambayo wanatumia wananchi au maeneo ya makazi au mahali pa ibada au hospitali au shule.

Leseni ya hoteli.

**29.** Leseni ya hoteli imtaruhusu mwenye leseni hiyo kumuuzia vileo vinavyolewesha mteja wake ambavyo vitanywewa ndani ya hoteli hiyo kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii.

Leseni ya baa.

**30.**-(1) Leseni ya baa itamruhusu mwenye leseni hiyo kuuza rejareja vileo vinavyolewesha ambavyo vitanywewa hapo hapo kati ya saa kumi jioni na saa sita usiku.

(2) Mtu yeyote mwenye leseni ya baa ambaye atakwenda kinyume na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au atanyang'anywa leseni yake.

(3) Taasisi yoyote ambayo itakwenda kinyume na kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itakuwa imetenda kosa na ikipatikana na hatia, italipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi za Kitanzania au ikishindwa kulipa faini, mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo au kunyang'nywa leseni hiyo.

(4) Mtu yeyote atakayeonekana anatoka kwenye baa huku akiwa amechukuwa vileo atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi miwili.

Leseni ya duka la vileo.

**31.**-(1) Leseni ya duka la vileo itamruhusu mwenye leseni hiyo kuuza, kati ya saa mbili asubuhi na saa moja usiku, kwa jumla au reja reja, vileo vinavyolewesha ambavyo havijafunguliwa na viko katika hali yake kama vilivyoagizwa, ambavyo havitanywewa hapo dukani.

(2) Vileo vyote vinavyolewesha, vinavyonunuliwa au kuuzwa, kwa ajili ya kunywewa mbali na viliponunuliwa au kuuzwa, vitafunikwa visionekane kabisa kwa njia inayofaa ili kuzuia usumbufu na kulinda heshima ya watu wengine.

(3) Kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii, duka la vileo linajumuisha maduka yote yaliyopewa kibali au leseni kufanya biashara ya vinywaji vinavyolewesha ambayo hayana sifa ya kuwa baa, klabu au hoteli.

(4) Taasisi au mtu yeyote mwenye leseni ya duka la vileo vinavyolewesha, atauza vileo hivyo pale atakapopokea hati ya ununuzi iliyowekwa kutoka kwa mnunuzi na muuzaji atatoa hati ya uuzaji wa vileo iliyowekwa na Bodi kwa ajili ya mauzo hayo.

(5) Hati zote za ununuzi na uuzaji zilizotayarishwa na Bodi, zitatolewa baada ya malipo ya ada iliyowekwa.

(6) Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Tano au kifungo kisichopungua miezi minne.

(7) Endapo ikitokea taasisi imetenda kosa chini ya kifungu hiki, taasisi hiyo italipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tano au ikishindwa kulipa, mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo.

Leseni ya ghala.

**32.**-(1)Leseni ya ghala ya vileo itamruhusu mwenye leseni hiyo kuhifadhi vileo vinavyolewesha kwenye ghala hiyo kwa mujibu wa udhibiti na masharti yaliyowekwa na Bodi.

(2) Mtu yeyote ambaye atakwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Sita au kifungo kisichopungua miezi mitano.

(3) Endapo ikitokea taasisi imetenda kosa chini ya kifungu hiki, taasisi hiyo italipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Kumi au ikishindwa kulipa, mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo na kunyang'anywa leseni.

Kibali cha kuagiza.

**33.**-(1) Kibali cha kuagiza kitatolewa kwa waagizaji wasiozidi watatu kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo, muagizaji:

(a) awe ni mzanzibari;

(b) awe ni mlipa kodi;

(c) awe na ghala; na

(d) awe na gari ya kusambazia vinywaji hivyo.

(2) Mtu yeyote ambaye anaingiza vileo vinavyolewesha Zanzibar bila ya kibali, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atatumikia kifungo kisichopungua miaka miwili au atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tano na vileo vyote alivyokamatwa navyo vitachukuliwa na kushughulikiwa kama Bodi itakavyoona inafaa.

(3) Endapo ikitokea taasisi imetenda kosa chini ya kifungu hiki, taasisi hiyo itakapotiwa hatiani, italipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tano au ikishindwa kulipa, mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo au kunyang'anywa kibali chake.

Kibali cha usambazaji.

**34.**-(1) Kibali cha usambazaji kitamruhusu mwenye kibali hicho kusambaza vileo vinavyolewesha kutoka sehemu au eneo moja kwenda sehemu au eneo jengine ndani ya Zanzibar.

(2) Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au atatumikia kifungo kisichopungua miezi mitatu na vileo vyote alivyokamatwa navyo vitachukuliwa na kushughulikiwa kama Bodi itakavyoona inafaa.

(3) Taasisi yoyote ambayo itakwenda kinyume na masharti kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itakuwa imetenda kosa, na ikipatikana na hatia, italipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Tano au ikishindwa kulipa faini, mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo au kunyang'nywa kibali chake.

Utaratibu wa kuhifadhi vileo katika maeneo yaliyoruhusiwa.

**35.**-(1)Taasisi au mtu yeyote mwenye leseni haruhusiki kuuza vileo vinavyolewesha isipokuwa kwanza lazima kiwepo chumba maalum cha kuhifadhia vileo ndani ya jengo hilo ambacho kimekubaliwa na Bodi.

(2) Vileo vyote vya ziada ambavyo havihitaji kuonekana hadharani vitahifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhia.

(3) Kileo chochote kinacholewesha ambacho kitawekwa na kuhifadhiwa katika sehemu tofauti na chumba cha kuhifadhia, kitachukuliwa na Bodi na kushughulikiwa kama inavyoona inafaa.

(4) Kabla ya leseni yoyote kutolewa, Bodi inaweza kukagua jengo hilo na kuhitaji marekebisho ya kimuundo ya kama inavyoonekana inafaa kwa ajili ya uhifadhi unaotakiwa wa vileo vinavyolewesha.

(5) Ni marufuku kwa taasisi au mtu yeyote mwenye leseni kubadilisha au kuongeza sehemu yoyote ya eneo la biashara ya vileo lenye leseni bila ya idhini ya Bodi.

## SEHEMU YA NNE
## UWEZO NA WAJIBU WA MAAFISA

Mkaguzi na Maafisa wa Bodi.

**36.** Mkaguzi au afisa aliyeidhinishwa na Bodi atakuwa na uwezo wa kufanya ukaguzi katika eneo la biashara ya vileo katika muda wowote na atapaswa kuwasilisha taarifa hizo za ukaguzi katika Bodi na Mamlaka ya Serikali za Mitaa husika.

Ukaguzi.

**37.**-(1) Mkaguzi au afisa yoyote wa Bodi, kwa madhumuni ya utekelezaji wa Sheria hii, katika muda wote, ataweza kuingia sehemu yoyote iliyotolewa leseni chini ya Sheria hii au mahala popote ambapo mtu aliyepewa leseni anafanya biashara yake.

(2) Endapo Mkaguzi au afisa wa Bodi yeyote ataingia kwenye jengo lolote kwa mujibu wa vifungu vya Sheria hii, basi anaweza:

(a) kumuagiza mwenye leseni ya eneo hilo kutoa kitabu, taarifa, nyaraka, kumbukumbu au kitu chochote ambacho aliyepewa leseni anapaswa kuweka chini ya masharti ya Sheria hii;

(b) kukagua kitabu, taarifa, nyaraka, kumbukumbu au kitu chochote na kuchukua nakala ya kitabu, taarifa, nyaraka, kumbukumbu au kitu chochote;

(c) kumtaka mwenye leseni au mtu yeyote aliyeajiriwa hapo kujibu maswali yanayohusiana na kitabu, taarifa, nyaraka, kumbukumbu au kitu chochote kilichoingizwa kwenye kumbukumbu, daftari au nyaraka yoyote;

(d) baada ya ukaguzi, kuchukua kitabu, taarifa, nyaraka, kumbukumbu au kitu chochote, ikiwa kwa maoni yake ni muhimu kwa ushahidi dhidi ya kosa lolote chini ya Sheria hii;

(e) kuagiza kontena, bahasha au kitu chengine chochote katika eneo hilo kufunguliwa;

(f) kwa gharama za mwenye leseni, kufungua na kuchunguza kifurushi chochote, vifaa au bidhaa yoyote katika eneo hilo; na

(g) kuchukuwa na kuzuia bila malipo, sampuli yoyote kama akiona ni muhimu katika utekelezaji wa majukumu yake;

(3) Iwapo, Mkaguzi au afisa wa Bodi anayefanya kazi chini ya masharti ya Sheria hii, amekumbana na kizuizi kuingia kwenye eneo la mwenye leseni ambapo mwingizaji anafanya biashara zake au kwenye eneo la mtu anayefanya biashara na mtu mwenye leseni au kukagua vifaa vilivyopo katika eneo hilo, anaweza, katika muda wowote, kuingia katika eneo hilo na kufungua vifaa hivyo kwa utaratibu au kwa kutumia nguvu kama ataona inafaa.

(4) Endapo, akiingia kwenye majengo yoyote yaliyoruhusiwa kwa leseni, vileo vyoyote ambavyo vimehusika kwenye kosa lolote lililotendeka chini ya Sheria hii vitataifishwa.

Matumizi mabaya ya mamlaka.

**38.** Afisa au mtu yeyote ambaye ameajiriwa kudhibiti makosa chini ya Sheria hii au Kanuni zilizotungwa endapo:

(a) akila njama kuzuia au kusambaza vifaa au akifanya makubaliano yoyote kusambaza au kuruhusu chombo au njia nyengine yoyote ya uchukuzi kusambaza vileo au kuruhusu vileo ambavyo vinatakiwa vizuiwe; au

(b) akipokea, akikubali kupokea au akijaribu kuchukua rushwa, malipo ya fadhila au hidaya ili kupuuza au kudharau majukumu yake; au

(c) kupanga au kula njama na mtu yeyote kufanya jambo au tendo lolote kinyume na Sheria hii au kiyume na utekelezaji wa majukumu yake;

atakuwa ametenda kosa dhidi ya Sheria hii na akipatikana na hatia, atatumikia kifungo kisichopungua miaka mitatu au kulipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Sita za Kitanzania.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI YA FEDHA

Fedha za Bodi.

**39.**-(1) Fedha na vyanzo vya mapato ya Bodi yatatokana na:

(a) fedha ambazo zitatolewa na Serikali kwa ajili ya shughuli za Bodi;

(b) kiasi chochote cha fedha kitakachopatikana kutokana na michango na kupitishwa na Bodi kwa kushauriana na Waziri; na

(c) fedha yoyote, ada, faini au adhabu na tozo yoyote ambayo hulipwa au kutolewa kwa Bodi kwa jambo lolote chini ya Sheria hii na Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii.

(2) Fedha zitatumika kutekeleza majukumu ya Bodi.

Hesabu na ukaguzi.

**40.**-(1) Bodi itaweka kumbukumbu sahihi za hesabu na taarifa nyengine za fedha na kumbukumbu nyengine kwa namna itakavyoidhinishwa na Waziri.

(2) Hesabu za Bodi zitakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

## SEHEMU YA SITA
## MASHARTI YA ADHABU

Makosa ya mtu aliyekatazwa.

**41.**-(1) Mtu aliyekatazwa haruhusiwi kuingia katika eneo lolote ambalo limepewa au lenye leseni ya vileo vinavyolewesha ndani ya Zanzibar.

(2) Vileo vyovyote vinavyolewesha ambavyo mtu aliyekatazwa atakutwa navyo vitachukuliwa na polisi au afisa yeyote aliyeidhinishwa chini ya Sheria hii.

(3) Mtu yeyote aliyekatazwa ambaye anakiuka masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini au atatumikia kifungo kilichotajwa katika kifungu cha 43(3) cha Sheria hii.

Makosa ya leseni.

**42.**-(1) Mwenye leseni itakuwa ni marufuku:

(a) kumruhusu mtu aliyekuwa ameshalewa kupita kiasi, kuingia katika eneo la biashara ya vileo na kulewa tena;

(b) kuruhusu eneo lake la biashara kufanywa kuwa danguro au kuwa ni mahali panapofanywa vitendo vya ukahaba;

(c) kufungua kwa ajili ya kuuza vileo vinavyolewesha kinyume na wakati ulioruhusiwa kwenye leseni yake;

(d) kuruhusu watu wengine ambao hawaruhusiki kusimamia au kuendesha biashara hiyo bila ya kibali kutoka kwenye Bodi;

(e) kuruhusu au kuingiza watu ambao hawaruhusiwi kuingia katika eneo hilo chini ya Sheria hii; au

(f) kumuuzia au kumpa au kuruhusu kuuziwa au kumpa mtu aliyekatazwa, vileo vinavyolewesha.

(2) Mtu yeyote mwenye leseni ambaye atakwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atanyang'anywa leseni yake au atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au atatumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miezi sita.

Amri ya kuzuia.

**43.**-(1) Bodi inaweza kutoa amri ya kuzuia kumuuzia, kununua, kuonekana na ulevi au kutumia vileo vinavyolewesha, mtu yeyote ambaye imethibitishwa kuwa na tabia ya kulewa kupita kiasi au mwenye sifa au tabia mbaya, kwa kipindi kisichopungua mwaka mmoja.

(2) Bodi itatoa taarifa ya zuio hilo kwa Waziri na kwa kila mwenye leseni kwa njia yoyote ile ambayo itaona inafaa.

(3) Mtu yeyote ambaye atakiuka amri ya kuzuia iliyotolewa na Bodi, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atatumikia kifungo kisichopungua miezi sita au kulipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja na vileo vyote alivyokamatwa navyo vitachukuliwa na kushughulikiwa kwa namna ambayo Bodi itaona inafaa.

(4) Endapo ikitokea taasisi imetenda kosa hilo dhidi ya kifungu hiki, taasisi hiyo italipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au ikishindwa kulipa, mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo na kunyang'anywa leseni.

(5) Taasisi au mtu yeyote ambaye hakuridhika na maamuzi ya Bodi chini ya kifungu hiki, anaruhusiwa kukata rufaa kwa Waziri, na maamuzi ya Waziri yatakuwa ni maamuzi ya mwisho.

Watu wasioruhusika kujishughulisha na biashara au muamala wa vileo.

**44.**-(1) Ni marufuku kwa taasisi au mtu yeyote mwenye leseni au kibali kumuajiri au kumshirikisha mtu yeyote aliyekatazwa kufanya shughuli au biashara ya vileo.

(2) Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya kifungu hiki, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au atatumikia kifungo kisichopungua miezi miwili.

(3) Endapo ikitokea taasisi imetenda kosa hilo dhidi ya kifungu hiki, taasisi hiyo italipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au ikishindwa kulipa mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo na kunyang'anywa leseni.

Kuuza au kuweka kwenye ghala bila ya leseni.

**45.**-(1)Mtu yeyote ambaye atauza au kuweka kwenye ghala vileo vinavyolewesha bila **ya** leseni atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi sita.

(2) Endapo ikitokea taasisi imetenda kosa chini ya kifungu hiki, taasisi hiyo italipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au ikishindwa kulipa mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo.

Kutumia nyaraka za uongo.

**46.**-(1) Taasisi au mtu yeyote ambaye ni mmiliki au anatengeneza, anasaini au anathibitisha nyaraka za uongo, hati ya ununuzi au uuzaji au hati nyengine za uongo, kwa madhumuni ya kukwepa au kuvunja masharti ya Sheria hii, atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia, atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au kifungo kisichopungua miezi sita.

(2) Endapo ikitokea taasisi imetenda kosa chini ya kifungu hiki, taasisi hiyo italipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Milioni Moja au ikishindwa kulipa mali za taasisi hiyo zilizopo Zanzibar zitakamatwa na kuuzwa kwa mnada ili kulipa faini hiyo.

Mahakama kuidhinisha hukumu.

**47.** Mahakama itapeleka katika Bodi na mamlaka ya serikali za mitaa husika, nakala ya hati ya hatia ya leseni au kibali iliyoidhinishwa.

Hukumu ya papo kwa papo.

**48.**-(1) Bodi inaweza kutoa hukumu ya papo kwa papo kwa makosa yaliyotendwa na taasisi au mtu yeyote dhidi ya Sheria hii au Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii na kusimamiwa na mamlaka ya serikali za mitaa ikiwa taasisi au mtu huyo:

(a) amekubali kwa maandishi kwamba ametenda kosa na atachukuwa tahadhari na hatorudia tena kufanya kosa hilo; na

(b) atalipa fedha nyengine anazodaiwa chini ya Sheria hii au Kanuni zake.

(2) Ikiwa faini iliyowekwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki haijalipwa, Bodi itafungua kesi Mahakamani dhidi ya taasisi au mtu huyo.

(3) Faini iliyotozwa na Bodi chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, haitochukuliwa kuwa ni kutiwa hatiani dhidi ya kosa lililodaiwa kwa masharti tu kwamba fedha zimelipwa kamili; hakuna mashtaka ambayo yatafunguliwa dhidi ya kosa hilo.

Adhabu ya Jumla.

**49.** Mtu yeyote ambaye atakiuka kifungu chochote cha Sheria hii au Kanuni yoyote itakayotungwa chini ya Sheria hii, na ambayo adhabu yake haijaainishwa, akitiwa hatiani atalipa faini isiyopungua Shilingi za Kitanzania Laki Moja au kifungo kisichopungua miezi mitatu.

## SEHEMU YA SABA
## MASHARTI YA JUMLA

Uwezo wa Waziri kutoa maelekezo kwa Bodi.

**50.**-(1) Kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, Waziri anaweza kutoa maagizo ya jumla kwa Bodi yanayohusu utekelezaji wa kazi na shughuli za Bodi.

(2) Bodi itayazingatia maagizo yote yaliyotolewa na Waziri.

Kinga dhidi ya kushitakiwa.

**51.** Hakuna afisa au mtu yeyote aliyeidhinishwa chini ya Sheria hii ambaye atashitakiwa kwa kesi ya jinai au madai kwa jambo au kitendo chochote alichokifanya kwa nia njema katika utekelezaji wa majukumu yake na uwezo aliopewa chini ya Sheria hii.

Kanuni.

**52.** Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa masharti ya Sheria hii.

Kufutwa.

**53.** Sheria ya Vileo, Sura ya 163 ya mwaka 1928 pamoja na marekebisho na kanuni zake zilizotungwa zimefutwa.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 6 Aprili, 2020.

..........................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***